



22110298



International Baccalaureate®  
Baccalauréat International  
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Monday 16 May 2011 (morning)

Lundi 16 mai 2011 (matin)

Lunes 16 de mayo de 2011 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.

*Jibu swalii moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanze huohuo ambaa umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nydingi.*

### Tamthilia

1. Kwa kuzingatia kazi mbili kutoka kwa angalau waandishi wawili uliojitayarishia jadili mbinu tofauti wanazozitumia katika kuwakuza wahusika wao na uonyeshe wamefaulu kwa kiwango kipi katika kutekeleza wajibu huu.
2. Ni kwa kiwango kipi na njia zipi waandishi wa kazi mbili kutoka kwa angalau waandishi wawili tofauti uliojitayarishia wanavyoonyesha uhusiano uliopo katika ya mpangilio au ploti za kazi zao?

### Riwaya

3. Jadili tofauti zinazojitokeza katika kukuza maudhui katika kazi mbili za waandishi tofauti ulizozisoma. Onyesha ni kwa nini baadhi ya waandishi hawa wanatofautiana katika mitazamo yao.
4. Jadili kwa kina vile maudhui ya haki za watoto yanavyokuzwa na waandishi wawili katika kazi tofauti na uonyeshe tofauti katika mitazamo yao.

### Ushairi

5. Kwa kuzingatia mashairi kutoka kwa washairi wawili uliojitayarishia jadili jinsi wanavyoshabihiana katika uteuzi wa maudhui na uonyeshe jinsi uteuzi huu unavyoathiriwa na jamii na matukio wanamojikuta.
6. Kwa kuzingatia kazi mbili kutoka kwa washairi wawili tofauti uliojitayarishia, jadili vile mbinu za istiara na methali zinavyoendelezwa na uonyeshe ni kwa kiasi kipi waandishi wa kazi hizi wanavyofaulu katika kutekeleza ukuzaji wa mbinu hizi.

### **Riwaya za mapenzi**

7. Riwaya za mapenzi zinaleta ukinzano kati ya shauku inayoletwa na mahitaji ya kimwili na uwajibikaji katika jamii. Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizozisoma na uonyeshe jinsi hali hizi mbili zinavyoendelezwa kwa njia mwafaka.
8. Siri na kuva nyuso mbili katika mapenzi kumesababisha kusabalatika kwa ndoa na uhusiano wa dhati. Jadili vile siri na uwongo zinavyokuzwa na kuwasilishwa kwenye kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia.

### **Maswala ya ujumla**

9. Fasihi hurembesha na kujumuisha tajriba katika jamii. Jadili ukizingatia angalau kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia vile ukweli wa msemo huu unavyoshamiri na kuendelezwa katika jamii.
10. Kusoma kazi ya fasihi ni njia moja wapo ya kukuza mitazamo tofauti katika vipengele tofauti. Fafanua kauli hii huku ukizingatia angalau kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizojitayarisha.
11. Onyesha vile wanafasihi wa kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili ulizojitayarishia wanavyoyakuza maudhui ya ugawaji wa raslimali na ujadili na uonyeshe jinsi ugawaji huu unavyoendeleza au kubomoa maadili ya kijamii.
12. Onyesha vile fasihi inavyohusu ukinzani, mivutano na mitafaruku ya kijamii na uonyeshe ukizingatia kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia jinsi mitafaruku hii inavyojitokeza na inapitishwa na mwandishi kwa njia ipi.